"Waziri" maana yake ni Waziri mwenye dhamana, ya. mambo yanayohusika na kuendeleza ardhi,

"mpima ardhi" maana yake ni mtu aliyehitimu baada. ya mafunzo na, mazoezi akapata. elimu, maarifa na ujuzi kiasi cha, kumwezesha kutekeleza fani ya-

(a) kukagua hesabu zinazohusika na. matumizi ya ardhi, kukagua hali na. ubora, wa; ardhi au haki ya kumiliki ardhi au majengo, na kukadiria au kupima thamani ya ardhi kwa ajili ya kuandaa matumizi bora, uuzaji, ununuzi, uwekaji wa. rehani, bima. au utayarishaji wa mipango ya kuendeleza ardhi; au

(b) kuchunguza na kutumia, vipimo maalum vya kupimia sehemu yoyote ya. nchi na. kupima hali na, ubora wa ardhi, eneo lake na mambo mengineyo kwa ajili ya-

(i) kuweka mipaka. na mambo mengineyo yanayohitajika kwa. madhumuni ya. kuandikisha haki ya, kumiliki ardhi;

(ii) kufanya, maandalio ya, upimaji na uchoraji wa ramani;

(iii) kuonyesha kwenye ramani umbile na hali ya sehemu yoyote ya, nchi,.

(iv) kutayarisha. habari na. taaria zinazohitajika kwa, ajili ya ramani za majengo na shughuli za ujenzi kwa jumla;

(v) kuonyesha kwenye ramani. takwimu na mambo mengineyo maalum, na,

maana, ya maneno hayo ifahamike kuwa itatumika pia kwa yeyote anayefanya kazi kama, mthamini wa ardhi na. mtaalam wa uchumi katika shughuli za kuendeleza ardhi;

"daftari" maana yake ni daftari la wapima ardhi litakalowekwa na Halmashauri kwa madhumuni ya Sheria hii;

"Katibu" maana yake ni Katibu wa Halmashauri aliyeteuliwa kwa mujibu wa fungu la, 7.

### SEHEMU YA PILI

#### KUANZISWHA KWA HALMASHAURI NA MASHARTI KUHUSU UANDIKISHAJI WA WIPIMA ARDHI

Kuanzishwa  
kwa Hal-  
mashauri

3. Sheria hii inaanzisha Halmashauri ambayo itaitwa Halmashauri ya Taifa ya Wapima. Ardhi nayo itakuwa na mamlaka ya kusimamia, kwa mujibu wa, Sheria, hii, tabia ya. wapima ardhi pamoja na mwenendo katika. utendaji wa. kazi zinazohusika na taaluma. yao.

Muundo wa  
Halmashauri,  
muda wa  
wajumbe wa  
kushika  
madaraka.  
n.k.

4,(1) Halmashauri itakuwa na wajumbe wasiopungua sita wala, kuzidi wanane na Waziri atamteua mwenyekiti kutoka. miongoni mwa wajumbe atakaowatena, kwa mujibu wa kifungu cha 2 (a).

(2) Wajumbe watakuwa-

(a) wapima ardhi walioandikishwa watatu ambao ni watumishi wa Serikali. watakaoteuliwa na Waziri;

(b) wapima ardhi walioandikishwa watatu ambao si watumishi wa Serikali, watakaoteuliwa na Waziri; na,

(c) watu wengine wasiozidi wawili watakaoteuliwa na Waziri.;

Isipokuwa kwamba watu wa kwanza watakaoteuliwa kwa mujibu wa fasili ya (a) na (b) itabidi wawe watu ambao Waziri anaona wanastahili kuandikishwa kwa mujibu wa fungu la 9 (1).

(3) Mjumbe atashika madaraka kwa muda ule utakaotajwa wakati atakapoteuliwa, au kama muda huo hautatajwa, basi kwa muda wa miaka mitatu tangu siku ile atakapoteuliwa na muda huo ukimalizika aweza kuteuliwa tena.

(4) Nafasi ya mjumbe itakuwa wazi ikiwa-

(a) mjumbe Ataondolewa katika madaraka kwa kufuta uteuzi wake; au

(b) mjumbe atajiuzulu; au

(c) mjumbe atafariki.

(5) Mjumbe aweza kujiuzulu kwa kutoa taarifa kwa maandishi kwa Waziri, na tangu siku ile iliyotajwa kwa ajili hiyo katika hiyo taarifa, au kama hakuna siku maalum iliyotajwa, basi kuanzia siku ile taarifa hiyo ya kujiuzulu itakapotolewa na Waziri huyo mjumbe atakoma kuwa mjumbe.

**5. Bila ya kuathiri masharti mengineyo ya Sheria hii. kazi za Halma. shauri zitakuwa-**

(a) kuweka daftari kwa ajili ya kuandikisha wapima ardhi kwa mujibu wa masharti ya Sheria hii;

(b) kufikiria maombi ya kutaka kuandikishwa kama mpima ardhi na kupitisha, uamuzi wake;

(c) kusimamia tabia ya wapima ardhi pamoja na mwenendo wao katika utendaji wa shughuli zao zinazohusika na taaluma ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi.

(d) kueneza na kukuza taaluma ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi-

(e) kutoa nafasi au vifaa kwa ajili ya mafunzo kuhusu taaluma ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi, na kuhimiza utafiti na matumizi ya elimu itokanayo na shughuli za utafiti katika kukuza taaluma ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi;

(f) kupima viwango vya elimu, maarifa na ujuzi vinavyohitajika kwa ajili ya kutimiza masharti ya kuandikishwa kwa mtu yeyote kama mpima ardhi kwa mujibu wa Sheria hii;

- (g) kustawisha ushirikiano miongoni mwa wapima ardhi na kati ya Halmashauri na vyombo vingine au mashirika mengine, bila ya kujali kama watu waliomo katika vyombo hivyo au mashirika hayo wanashughulika na kazi ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi au sivyo;
- (h) kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Serikali na vyombo vingine vya Umma juu ya mambo yanayohusika na kazi ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi;
- (i) kuwasaidia wananchi katika kutekeleza masilahi yao yanayotokana au kuhusika na shughuli za kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi;
- (j) kutekeleza madaraka mengineyo yoyote yatakayotolewa kwa Halmashauri na Sheria nyingine yoyote au kutekeleza shughuli zozote zitakazoonekana zinafaa kwa ajili ya utendaji bora wa kazi za Halmashauri kwa mujibu wa Sheria hii.

Uwezo wa Halmashauri wa kumsimamisha kazi au kumfuta mpima ardhi

**6.** Halmashauri yaweza, baada ya kufanya uchunguzi madhubuti na kwa kufuata masharti yatakayokuwemo katika Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa fungu la 27, kumsimamisha kazi au kumfuta kabisa mpima ardhi:

Isipokuwa kwamba kila mara Halmashauri itakapofanya uchunguzi kwa mujibu wa fungu hili itabidi impe huyo mpima ardhi anayehusika nafasi ya kutosha ya kujieleza kuhusu lawama zote zitakazotolewa juu yake.

Uteuzi wa Katibu na kazi zake

**7.**-(1) Waziri atamteua mtumishi wa Umma kuwa Katibu wa Halmashauri.

(2) Katibu atatekeleza kazi anazohusika nazo zilizotajwa katika Sheria hii na pia atatekeleza shughuli nyingine zote atakazoagizwa mara kwa mara na Waziri au Halmashauri

Daftari la orodha ya wapima ardhi

**8.**-(1) Mapema iwezekanavyo baada ya Halmashauri kukubali kuandikisha mtu yeyote kama mpima, ardhi. Katibu ataandika katika daftari maelezo yafuatayo kuhusu kuhusu-

- (a) jina lake na anwani yake;
- (b) tarehe ya kuandikishwa kwake;
- (c) sifa zake zinazohusika na masharti ya kuandikishwa na maelezo yanayoonyesha kaina ameandikishwa kwa mujibu wa fungu lipi la Sheria hii;
- (d) maelezo mengine yoyote yatatakayo takiwa mara kwa mara na Halmashauri.

(2) Katibu ataandika katika daftari mabadiliko yoyote yatakayofanywa kuhusu maelezo yaliyoandikishwa kwa mujibu wa kifungu cha (1).

(3) Katibu aweza, kwa idhini ya Halmashauri, kusahihisha makosa yoyote yaliyomo katika daftari au hati nyingine yoyote yenye nakala ya maelezo yaliyomo kwenye daftari.

9.-(1) Bila ya kuathiri masharti yoyote yatayokuwamo kwenye Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa fungu la 27 kuhusu utaratibu wa kumsimamisha kazi mpima ardhi au kumfuta kabisa, mtu atakuwa na haki ya kuandikishwa kwa mujibu wa fungu hili, na kutoa huduma kwa malipo kama mpima ardhi ikiwa mtu huyo amepeleka maombi ya kutaka kuandikishwa na iwapo mtu huyo--

- (a) ana shahada ambayo inatambuliwa na Halmashauri kuwa ni ushahidi thabiti kwamba ana elimu, maarifa na ujuzi kiasi cha kumwezesha kutekeleza fani ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi; au
- (b) baada ya kupata shahada yake, amechukua hatua za kujipatia maarifa na mazoezi ya kazi kufuatana na masharti yoyote yaliyomo kwenye Kanuni zilizowekwa na Waziri, baada ya kushauriana na Halmashauri, kwa mujibu wa fungu la 27.

(2) Halmashauri yaweza kumtaka mtu yoyote aliyepeleka maombi ya kutaka kuandikishwa kwa mujibu wa fungu hili airidishe Halmashauri kwamba tabia yake kwa jumla na pia mwenendo wake katika utendaji wa kazi zake za kitaalamu ni bora na kwamba anastahili kuandikishwa.

10.-(1) Bila ya kuathiri masharti yoyote yatakayokuwemo kwenye Kanuni zitakazowekwa kwa mujibu wa fungu la 27 kuhusu waratibu wa kumsimamisha kazi mpima ardhi au kumfuta kabisa, mtu yeyote ambaye hana haki ya kuandikishwa kwa sababu moja tu kwamba baada ya kupata shahada yake hakuwahi kujipatia maarifa na mazoezi ya kazi kufuatana na masharti yaliyotajwa katika fungu la 9 (1) (b). atakuwa na haki ya kuandikishwa kwa mujibu wa fungu hili baada ya kupoleka rasmi maombi yake na kuiridhisha Halmashauri kuwa amepata nafasi ya kuajiriwa au mafunzo katika utumishi wa Umma au kwa watu au shirika la watu waliokubaliwa na Halmashauri kwa ajili ya kumwezesha kupata hayo maarifa na mazoezi ya kazi.

(2) Mtu aliyandikishwa kwa mujibu wa fungu hili atahesabiwa kuwa ana uwezo kamili wa kutekeleza shughuli zake zote za kitaalamu kwa muda wote atakapokuwa ameajiriwa au atakapokuwa anapata mafunzo kwa namna ilivyoolezwa katika kifungu cha (1), na katika muda huo atastahili kutumia, haki zote na kufaidi masilahi yote ya mpima, ardhi aliyeandikishwa, lakini hatakuwa na haki ya kutumia haki yoyote au kufaidi masilahi yoyote ambayo hayaambatani na kuajiliwa kwake au mafunzo yake kwa ajili ya, kujipatia maarifa na, mazoezi ya kazi.

(3) Mara tu mtu atakapoandikishwa kwa mujibu wa fungu la 9 kuandikishwa kwake kwa mujibu wa fungu hili kutakoma kuwa na, nguvu ya kisheria na hakutatambuliwa tena.

11.-(1) Iwapo mtu atairidhisha Halmashauri-

- (a) kwamba haishi Tanganyika;
- (b) kwamba ameajiriwa au anakusudia kuajiriwa Tanganyika kama mpima ardhi kwa madhumuni ya kutekeleza mkataba maalum wa kuajiriwa-. na

Uandikishaji  
wa muda

(c) kwamba wakati huo anapotoa maombi yake ya. kutaka kuandikishwa anafanya kazi kama, mpima, ardhi au kwamba kabla hajafika Tanganyika alikuwa anafanya kazi kama mpima ardhi na kwamba anastahili kuandikishwa kwa. mujibu wa, fungu la 9, basi Halmshauri yaweza, ikiridhika kuwa tabia yake kwa, jumla na mwenendo wake katika. utendaji wa, kazi za. kitaalamu ni bora na kwamba anastahili kuandikishwa., kuagiza kuwa aandikishwe kwa mujibu wa, fungu bili kwa muda wote atakapokuwa anatekeleza huo mkataba maalum wa kuajiriwa au kwa muda wowote mwingine utakaotajwa na Halmashauri.

(2) Halmashauri yaweza, kumtaka mtu yeyote aliyepeleka maombi ya kutaka kuandikishwa kwa mujibu wa fungu hili afike mbele ya Halmashauri kwa ajili ya kuhojiwa au awasilishe hati zinazohusika na, kazi zake -au mkataba wake wa kuajiriwa kama mpima ardhi.

(3) Kuandikishwa, kwa, mtu kwa mujibu, wa. fungu hili kutakuwa na nguvu ya kisheria. na, kutatambuliwa, kwa muda, ule tu wa mkataba maalum wa, kuajiriwa au muda ule mwingine uliotajwa na Halmashauri na mara. tu muda. huo utakapomalizika au akikoma kuajiliwa kwa huo mkataba. maalum kuandikishwa. kwake hakutakuwa. na nguvu ya kisheria. na, hakutatambuliwa tena. Iwapo kuna mashaka, yoyote, kuhusu kumalizika kwa muda uliotajwa, na, Halmashauri au kumalizika kwa, wajibu wake wa kutekeleza. huo mkataba maalum wa kuajiriwa, basi uamuzi wa Halmashauri juu ya suala hilo utakuwa wa mwisho.

(4) Mpima ardhi aliyeandikishwa. kwa mujibu wa fungu hili atahesabiwa. kaina ameandikishwa. kwa, mujibu wa fungu la 9 kuhusu shughuli zote atakazotekeleza katika muda wote wa, huo mkataba maalum wa kuajiriwa au muda wote uliotajwa na, Halmashauri, lakini hatahesabiwa hivyo kuhusu shughuli nyingine zozote ambazo hazihusiani na huo mkataba maalum wa kuajiriwa.

Haki za mpima ardhi aliyeandikishwa

**12.** Kwa wakati wote ambapo kuandikishwa kwake kuna nguvu ya kisheria. na kunatambuliwa kila, mpima ardhi aliyeandikishwa atakuwa na, haki ya kuitwa, mpirna ardhi mtaalam na kutumia pamoja na jina lake maelezo ya kitaalam yafuatayo-

(a) kwa. mpima. ardhi aliyeandikishwa kwa. mujibu wa fungu la 9, "Mpima Ardhi Aliyeandikishwa Kwa. Ukamilifu"

(b) kwa mpima, ardhi aliyeandikishwa kwa. mujibu wa, fungu la. 10. "Mpima Ardhi Aliyeandikishwa Kwa Mazoezi";

(c) kwa mpima ardhi aliyeandikishwa, kwa, mujibu wa fungu la 11, "Mpima, Ardhi Aliyeandikishwa Kwa Muda"

au ufupisho wowote wa maelezo hayo utakaokubaliwa na Halmashauri.

Utangazaji wa mambo yaliyoandikishwa na orodha ya wapima ardhi

**13.**-(1) Mapema iwezekanavyo baada. ya mpima. ardhi kuandikishwa. Katibu atachapisha kwenye *Gazeti la Serikali* maelezo yaliyoandikwa katika daftari kuhusu kila mpima ardhi na, kwa kufuata maagizo yoyote yatakayotolewa na Halmashauri, aweza kuchapisha kwenye *Gazeti la Serikali* masahihisho au taarifa ya ufutaji wa maelezo yoyote yaliyoandikishwa katika daftari.

(2) Katibu atachapisha kwenye *Gazeti la Serikali*, angalau mara moja kila mwaka, orodha ya maelezo yote yaliyoandikwa katika daftari kuhusu wapima ardhi wote ambao majina yao yalikuwa bado yamo katika daftari mwishoni mwa mwaka uliopita.

**14.**-(1) Utangazaji wa maelezo yaliyoandikwa katika daftari kwa kuchapisha kwenye *Gazeti la Serikali* kwa mujibu wa fungu la 13 utakuwa ni ushahidi wa kutosha, isipokuwa kama imethibitishwa vinginevyo, kwamba watu waliotajwa katika taarifa hiyo wameandikishwa kwa mujibu wa Sheria hii, na iwapo taarifa iliyotangazwa hivyo itaonyesha kwamba jina la mtu yeyote limefutwa katika daftari, au iwapo jina la mtu yeyote halitakuwemo katika taarifa kama hiyo, basi hali hiyo ya jina kufutwa au kutokuwemo itakuwa m ushahidi wa kutosha, isipokuwa kama imethibitishwa vinginevyo, kwamba mwenye jina hilo hakuandikishwa au kwamba kuandikishwa kwake kumekoma kuwa na nguvu ya kisheria na hakutambuliwi, tena.

Utangazaji ni ushahidi wa uandikishaji

(2) Daftari, orodha na kila nakala ya maelezo yaliyomo katika daftari au orodha inayoonyesha kuwa imethibitishwa kwa sahihi ya Katibu itabidi ikubaliwe na mahakama zote na vyombo vingine vyote vyenye mamlaka ya kupokea ushahidi kwamba m ushahidi wa kutosha, isipokuwa kama imethibitishwa vinginevyo, kuwa maelezo yote yaliyomo katika hilo daftari au hiyo orodha au nakala ni ya kweli na sahihi.

**15.** Iwapo Katibu ataagizwa na Halmashauri kuchukua hatua kama hiyo, basi itambidi kumwomba mpima ardhi aliyeandikishwa yeyote, kwa kumpelekea barua ya rejesta akitumia anwani yake anayojijua, atoe maelezo yoyote yatakayotakiwa na Halmashauri kuhusu shughuli za huyo mpima ardhi.

Katibu aweza kuiagiza apatiwe maelezo

## SEHEMU YA TATU

### RUFAA

**16.**-(1) Sheria hii inaanzisha Baraza la Rufaa ambalo litasikiliiza na kuamua mashauri ya rufaa za kupinga uamuzi wowote wa Halmashauri unaohusika na uandikishaji wa wapima ardhi.

Baraza la Rufaa

(2) Baraza la Rufaa litakuwa na wajumbe wafuatao-

- (a) Mwenyekiti ambaye atateuliwa na Waziri;
- (b) mwanasheria aliyeajiriwa katika Ofisi ya Mwanasheria Mkuu wa Serikali, ambaye atateuliwa kuwa mjumbe na Mwanasheria Mkuu wa Serikali, naye atakuwa ndiye Makamu wa Mwenyekiti;
- (c) watu wengine wasiozidi watatu watakaoteuliwa na Waziri.

**17.**(1) mtu yeyote ambaye hataridhika na uamuzi wowote wa Halmashauri juu ya jambo lolote linalohusika na uandikishaji wake kwa mujibu wa Sheria hii aweza kukata rufaa mbele ya Baraza la Rufaa akipinga uamuzi huo na katika rufaa kama hiyo Baraza la Rufaa litakuwa na mamlaka ya kupitisha uamuzi na kutoa maagizo yoyote yanaoonekana yatatimiza haki kwa wote wanaohusika katika shauri hilo.

Rufaa za kupinga uamuzi wa Halmashauri

(2) Maagizo yote yatakayokuwemo katika uamuzi au amri ya Baraza la Rufaa yatakayotolewa kwa mujibu wa fungu hili yatakuwa ya mwisho na itabid yafuatwe na wote wanaohusika katika shauri hilo.

(3) Endapo kutakuwa na rufaa inayosikilizwa na Baraza la Rufaa ya kupinga uamuzi wa Halmashauri, basi Halmashauri yaweza kufika mbele ya Baraza la Rufaa, na kutoa maelezo yake juu ya shauri hilo na, kwa madhumuni ya kuliwezesha Baraza la Rufaa kutoa maagizo kuhusu nani atalipa gharama za shauri lililosikilizwa na Baraza, la Rufaa, Halmashauri itahesabiwa kama ni mmojawapo wa watu wanaohusika katika shauri hilo, na itahesabiwa hivyo bila kujali kama wakati shauri liliposikilizwa Halmashauri ilifika mbele ya Baraza la Rufaa au hapana.

(4) Waziri aweza kuweka Kanuni, kwa mujibu wa fungu la 27, za kueleza utaratibu wa kukata rufaa mbele ya Baraza la Rufaa, kutoa mamlaka kwa Baraza la Rufaa ya kupokea ushahidi zaidi katika shauri loloto linalosikilizwa, kutaja ada zitakazotozwa kwa ajili ya kukata rufaa na kueleza utaratibu wa kutoa taarifa kwa Halmashauri kuhusu rufaa zilizofikishwa mbele ya Baraza la Rufaa.

## SEHEMU YA NNE

### USIMAMIZI JUU YA SHUGHULI ZA WAPIMA ARDHI

Masharti ya kufanya kazi kama wapima ardhi

**18.**-(1) Baada ya kumalizika muda wa miezi sita tangu tarehe ya kuanza kutumika Sheria hii, au muda wowote wa nyongeza utakaotajwa na Waziri kwa mujibu wa kifungu cha (2), mtu yeyote ambaye hakuandikishwa kama mpima ardhi kwa mujibu wa Sheria hii-

- (a) atakayejidai kuwa mpima ardhi kwa maana iliyoelezwa katika Sheria hii; au
- (b) atakayejiita mpima ardhi mtaalamu na kutumia pamoja na jina lake maelezo ya kitaalamu yaliyotajwa katika fungu la 12 au atakayetumia jina, choo au maelezo ya kitaalamu ya namna nyingine yoyote kwa makusudi ya kuwafanya watu wamtambue au wamfikirie kuwa mpima ardhi mtaalamu; au
- (c) atakayejitambulisha kwa watu kama mpima ardhi au kama mtaalamu mwenye haki ya kufanya kazi kama mpima ardhi,

atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia mbele ya mahakama atastahili kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyoziidi shilingi Thelmathini elfu au kufungwa gerezani kwa muda usioziidi miaka mitano au adhabu zote mbili pamoja.

(2) Waziri aweza, kwa kutoa tangazo litakalochapishwa kwenye *Gazed la Serikali* kuongeza muda wa miezi sita, uliotajwa katika kifungu cha (1) kwa muda usioziidi miezi sita mingine, na muda huo wa nyongeza waweza kutajwa kwa ajili ya watu wote kwa jumla au kwa ajili ya mtu mmoja maalum au aina fulani maalum ya watu.

Mashirika yanayofanya kazi kama wapima ardhi

**19.**-(1) Ni marufuku kwa shirika la watu la aina yoyote kufanya kazi kama wapima ardhi ila kwa sharti kwamba kila mwanachama au kila mwenye hisa katika shirika hilo awe ameandikishwa kama mpima ardhi.

(2) Endapo mwanachama yeyote au mtu yoyote mwenyo hisa katika shirika la watu la. aina yoyote linalofanya kazi kama wapima ardhi atafariki, basi shirika. hilo laweza, bila ya kujali masharti ya kifungu cha, (1), kuendelea kufanya kazi kama. wapima ardhi mpaka, mashauri ya. mirathi ya huyo marehernu yatakapokamilika, na kwa madhumuni hayo wale watu wote watakaoendesha, mashauri hayo ya mirathi pamoja na warithi wa. marehemu watahesabiwa, kama wapima. ardhi walioandikishwa.

(3) Masharti ya, Sheria hii yasifahamike kuwa. yanatoa haki kwa shirika la watu la, aina. yoyote ya kuandikishwa kama, wapima. ardhi.

(4) Shirika la watu la, aina yoyote litakalofanya kazi kama. wapima ardhi kinyume cha masharti ya fungu hili litakuwa limetenda kosa na likipatikana na hatia mbele ya, mahakama litastahili kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi hamsini elfu.

**20.** Kwa madhumuni ya Sheria hii mtu atahesabiwa kuwa, anafanya kazi kama. mpima, ardhi ikiwa anatoa ada au ushuru wa. aina yoyote kwa huduma. anazotoa kama, mpima ardhi kwa mwajiri wake au kwa mtu mwingine yeyote aliyefanya, naye mapatano kuhusu huduma anazotoa.

Tafsiri ya  
"kufanya  
kazi kama  
mpima ardhi"

**21.** Mtu yeyote ambaye-

- (a) kwa udanganyifu, ataandikisha au atasababisha uandikishaji katika, daftari au nakala yoyote ya daftari maelezo yoyote ya uwongo au yasiyo sahihi; au
- (b) kwa. udanganyifu, atajiandikisha au atajaribu kujiandikisha au kumwandikisha mtu mwingine yeyote kama mpima ardhi; au
- (c) kwa makusudi, atatoa maelezo yoyote ambayo anajua ni ya uwongo au ya. kupotosha, kwa. madhumuni ya kujipatia masilahi yoyote kwa mujibu wa. Sheria. hii au kumwezesha mtu mwingine yeyote kupata. masilahi kama hayo,

Makosa  
yanayohu-  
sika  
na auandiki-  
shaji

atakuwa. ametenda kosa na akipatikana na, hatia, mbele ya mahakama atastahili kuadhibiwa kwa kutozwa faini isiyozidi shilingi elfu tano au kufungwa, gerehani kwa muda usiozidi miezi kumi na mbili au adhabu zote mbili pamoja.

**22.** Mtu hatashtakiwa mahakamani kwa ajili ya, kosa lolote kwa mujibu wa Sheria hii ila mpaka kipatikane kwanza kibali cha Mkurugenzi wa Mashtaka.

Kibali cha  
Mkurugenzi  
wa Mashtaka

## SEHEMU YA TANO

### MASHARTI MENGINEYO

**23.** Mjumbe yeyote wa Halmashauri, Katibu au mtu mwingine yoyote mwenye madaraka ya kutekeleza jambo lolote kwa mujibu wa Sheria hii akitenda jambo lolote kwa nia njema katika kutekeleza, madaraka yake kwa mujibu wa Sheria hii hatakuwa na lawama yoyote ya kustahili kuchukuliwa hatua za kisheria juu yake kutokana na jambo kama hilo.

Ukomo wa  
dhima ya  
wajumbe wa  
Halmashauri,  
Katibu n.k.

Taarifa ya mwaka

**24.** Kila, mwisho wa Mwaka, Halmashauri itatakiwa kutayarisha taarifa kuhusu shughuli za Halmashauri katika mwaka huo na, itawasilisha taarifa, hiyo kwa Waziri.

Msamaha

**25.-** Waziri waweza, kwa kutoa amri itakoyochapishwa kwenye *Gazeti la Serikali*, kumsamehe mtu yeyote au, kuwasamehe watu wa aina yoyote masharti yote ya Sheria, hii au sharti lolote kati ya hayo.

Sheria Ndogo za Halma-shauri

**26.-(1)** Halmashauri yaweza, kwa idhini ya Waziri, kutunga Sheria Ndogo kwa, ajili ya utekelezaji bora wa kazi zake kwa mujibu wa Sheria hii, na bila ya kuathin mamlaka hayo yaliyoelezwa kwa jumla, Halmashauri yaweza. kwa kutuima Sheria, Ndogo kama hizi,

- (a) kutaja aina za shahada ambazo zinatambuliwa na, Halmashauri kwa madhumuni ya, kumwezesha mtu yeyote mwenye shahada ya aina mojawapo kati ya hizo kuandikishwa kwa. mujibu wa Sheria hii;
- (b) kueleza kanuni zitakazotumika kama mwongozo kwa ajili ya, kudumisha tabia njema ya wataalam na mwenendo bora katika utekelezaji wa kazi ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi;
- (c) kueleza kanuni kwa ajili ya utaratibu wa kusimamia utekelezaji wa kati ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi;
- (d) kueleza utaratibu wa kutoa msaada kwa, wananchi katika, kutekeleza masilahi yao yanayotokana au kuhusika na shughuli za kupima, kuthamini na. kuendeleza ardhi;
- (q) kueleza jambo jingine lolote ambalo Halmashauri itaona linafaa. kwa ajili ya kurahisisha au kuendeleza utekelezaji bora. wa kazi na madaraka yake kwa mujibu wa Sheria hii.

(2) Sheria, Ndogo zote zitazotungwa na. Halmashauri kwa mujibu wa, fungu hili zitatakiwa zichapishwe kwenye *Gazeti la Serikali*.

Kanuni za Waziri

**27.** Waziri aweza. kuweka Kanuni kwa. ajili ya utekelezaji bora wa madhumuni na masharti ya Sheria hii, na bila. ya kuathiri mamlaka, hayo yaliyoelezwa kwa jumla, Waziri aweza, kwa kutumia Kanuni kama hizo-

- (a) kutaja aina za fomu zitakazotumika kwa ajili ya. maombi ya, kutaka kuandikishwa kama mpima. ardhi au maombi ya kutaka. kuandikishwa tena kwa mpima, ardhi ambaye jina lake lifi-futwe katika daftari, kueleza utaratibu wa kupeleka maombi ya aina mbali mbali na kutaja viwango vya ada zitakazotowza kwa ajili ya maombi au mambo mengineyo;
- (b) baada ya kushauriana na Halmashauri, kueleza masharti yaliyotajwa katika fungu la 9 (1) (b) yanayotakiwa yatimizwe na mtu yeyote anayetaka kujipatia maarifa na mazoezi ya kazi kwa ajili ya kupata haki ya kuandikishwa kama mpima ardhi;
- (c) kueleza utaratibu utakaotumika kwa ajili ya kuendesha shughuli za Halmashauri na utaratibu utakaofuatwa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya uchunguzi kwa mujibu wa Sheria hii;

- (d) kueleza utaratibu wa. kuiwezesha Halmashauri kuteua kamati za wajumbe wake na utaratibu wa, kuiwezesha Halmashauri kuwashirikisha katika kamati zake watu wengine wasio wajumbe wa Halmashauri;
- (e) kutaja shughuli zitazotekelezwa na Katibu pamoja na kazi zake zilizoolezwa katika Sheria hii;
- (f) kueleza kanuni zitakazotumika kwa ajili ya kuwasimamisha kazi au kuwafuta. kabisa wapima ardhi;
- (g) kueleza utaratibu utakaotumika kwa ajili ya. kukata, rufaa mbele ya Baraza, la Rufaa, kuhusu mambo yaliyoolezwa katika fungu la, 17(4)-;
- (h) kueleza jambo jingine lolote linalotakiwa. au kuruhusiwa kuelezwa katika Kanuni kwa, mujibu wa Sheria hii.

**28.**-(1) Bila, ya kuathiri masharti ya Sheria yoyote inayotumika kuhusu shughuli za kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi, Waziri aweza, kwa kutoa, maagizo yatakayotangazwa katika, *Gazeti la Serikali*, kuitaka Halmashauri au kumtaka mpima ardhi aliyeandikishwa yeyote au kuwataka wapima ardhi wa aina yoyote walioandikishwa kuzingatia, mambo yoyote yatakatajwa na Waziri kwa madhumuni ya kulinda au kuendeleza masilahi ya Umma na Halmashauri itakuwa na wajibu wa kuzingatia mambo hayo katika utekelezaji wa madaraka yake kwa mujibu wa Sheria hii, hali kadhalika kila mpima ardhi anayehusika atakuwa na wajibu wa kuzingatia mambo hayo anapofanya kazi kama mpima ardhi.

Maagizo ya mwongozo kuhusu misingi ma kanuni za kufanya kazi kama mpima ardhi

(2) Bila ya kuathiri mamlaka ya jumla yaliyoolezwa katika kifungu cha (1), Waziri aweza kutaja. mambo ya aina iliyolezwa katika kifungu hicho kwa, madhumuni ya-

- (a) kuanzisha na kutekeleza, utaratibu wa, kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi unaolingana na siasa ya, Jamhuri ya Muungano kuhusu matumizi bora. ya ardhi na shughuli zingine zinazoa-mbatana na matumizi ya ardhi;
- (b) kukuza shughuli za utekelezaji wa taaluma, ya kupima, kuthamini na kuendeleza ardhi kusudi utekelezaji wa taaluma hiyo ulingane na ufuata misingi ya siasa ya Ujamaa na Kujitegemea pamoia na kutimiza masilahi ya watu wa Jamhuri ya Muungano katika mambo ya kisiasa, uchumi na ustawi wa jamii.

(3) Maagizo yatakayotolewa na Waziri kwa mujibu wa fungu hili yatakuwa na nguvu kamili ya kisheria sawa na masharti yaliyomo katika Sheria hii.

Imepitishwa katika Bunge tarehe kumi na nane mwezi Januari, 1977.



Clerk of the National Assembly